DHULUMA ZA NYUMBANI NA COVID-19: JINSI MAKANISA YANAVYOWEZA KUCHUKUA HATUA

Mandy Marshall

Rasilimali ya pamoja kutoka Anglican Consultative Council na Anglican Alliance

ANGLICAN ALLIANCE
Development · Relief · Advocacy

ANGLICAN COMMUNION
IN OVER 165 COUNTRIES

Dibaji

Katika kipindi cha janga la COVID-19, nchi nyingi zimeshuhudia ongezeko la visa vya dhuluma za nyumbani na ongezeko la wanaume na wanawake wanaoomba msaada kupitia huduma ya namba ya simu ya kitaifa, endapo inapatikana.

Dhuluma za nyumbani bado ni baa lililofichika katika jamii zetu na katika makanisa, baa ambalo halishughulikiwi na badala yake huachwa tu. Dhuluma za nyumbani ni dhambi na zinaweza kusababisha kiwewe cha kudumu katika wale waliopitia masaibu hayo. Sisi kama Wakristo wito wetu ni kumpenda Mungu na kupendana sisi kwa sisi na kutunzana. Hii inamaanisha tuna wajibu wa kuhakikisha kila mtu anawajibika na tunashutumu udhalimu wakati tunapouona na mahali tunapouona ukitendeka. Nikikumbuka maazimio ya ACC 15:7 na 16:3, ambayo yanatuhimiza sote kukabiliana na dhuluma za nyumbani na dhuluma za kijinsia, ninapendekeza makala haya kwako ili yakuwezeshe kushughulikia dhuluma za kinyumbani katika kipindi hiki ambacho hali hii imeongezeka.'

iliyoandikwa na Askofu Mkuu
Dk Josiah Idowu-Fearon, Katibu Mkuu wa
Jumuiya ya Waanglikana

Utangulizi

Janga la COVID-19 limeathiri pakubwa na bado linaathiri pakubwa jamii ulimwenguni kote. Matokeo yake ni kuwa, serikali zinaweka mikakati mbalimbali ya kuudhibiti mlipuko huo. Baadhi ya mikakati hii, kama vile kujitenga ukiwa nyumbani, inaweza kuchangia ueneaji na uzito wa dhuluma za nyumbani na dhuluma za kijinsia.

Janga la COVID-19 limeathiri pakubwa na bado linaathiri pakubwa jamii ulimwenguni kote. Matokeo yake ni kuwa, serikali zinaweka mikakati mbalimbali ya kuudhibiti mlipuko huo. Baadhi ya mikakati hii, kama vile kujitenga ukiwa nyumbani, inaweza kuchangia ueneaji na uzito wa dhuluma za nyumbani na dhuluma za kijinsia.

Katika nchi nyingi, nambari za simu za Kitaifa zinazomwezesha mtu kupokea msaada zimeshuhudia kuongezeka kwa idadi ya simu zinazopigwa. Kinachosababisha dhuluma hizo si ile mikakati iliyowekwa na serikali, kwa kuwa wajibu na uamuzi wa kutekeleza dhuluma hizi unabaki kuwa wa yule mtendaji, hata hivyo mikakati hiyo inaweza kumzuia yule aliyedhulumiwa kupokea usaidizi au hata kujinusurisha na dhuluma hizo. Kuongezeka kwa hofu, wasiwasi na ukosefu wa hela unaweza kuyafanya mazingira hayo mabaya kuwa mabaya zaidi na dhuluma ikashamiri pasipo pingamizi zozote.

Kanisa lina nafasi nzuri katika jamii ya kuweza kuwa nuru na kimbilio katika wakati wa mahitaji na linaweza kuzifikia jamii wakati serikali haiwezi kuzifikia. Wito wetu wa Kikristo ni kupendana kama Kristo alivyotupenda na sikuwaacha watu wa mwili wetu na damu yetu. Stakabadhi hii ni mwongozo wa kuwaandaa viongozi wa kanisa na watu wanaokwenda kanisani (washirika) waweze kuchukua hatua juu dhuluma za nyumbani kulingana na njia inayofaa.

Mbinu ya TIMA ya **tambua, itikia, mtume** na **andika**, hutumika kama mfumo kwa ajili ya kuwasaidia manusura, pasipo kuondoa uwezo wa manusura wenyewe wa kuitikia na kukujulisha kile wanachohitaji vile vile. Mbinu ya TTOMPAP ya **tambua, tubu, ondoa, mtume, patana, andika** na **pitia** hutumika kama mfumo kwa wale wanaodhulumu ili waache dhuluma na wawajibikie matendo yao. Mwongozo huo unajumuisha utangulizi wa theolojia, ufafanuzi wa dhuluma ni nini na jinsi ilivyoenea, na kufuatiwa na hatua za kimatendo tunazoweza kuchukua, zikiwemo kuongea na wanaume, na kupigania mabadiliko. Maombi ni sehemu ya hatua tunazochukua, lakini manusura wa dhuluma wanahitaji usaidizi wa matendo na kushikwa mkono.

Katika stakabadhi hii yote, mdhulumu ataitwa 'mwanamume' na yule aliyedhulumiwa na mwathariwa ataitwa 'mwanamke'. Lengo la kufanya hivyo ni kuwakilisha jinsia inayotekeleza dhuluma zaidi. Kanuni za mbinu bora zaidi zilizoelezwa katika stakabadhi hii zinawafaa manusura wa dhuluma wa kiume pia na ni muhimu kutambua kwamba hili pia linatendeka katika jamii na hivyo tunapaswa kufungua macho kuona dalili zozote, ili manusura wa kiume waweze kusaidiwa pia. Neno manusura litatumika badala ya neno mwathirika ili kutambua uwezo wa wanawake kuweza kunusurika katika hali zao za sasa na pia wale ambao hawako tena na wapenzi wanaowadhulumu na wameweza kunusurika.

COVID-19

Ulimwengu unapitia nyakati ambazo haujawahi kuzipitia mbeleni kwa kuenea kwa janga la COVID-19, ambalo pia linajulikana kama Coronavirus, na nchi zinakabiliana na janga hili kwa njia tofauti tofauti.

Njia hizi zinajumuisha: kutokaribiana, kujitenga kibinafsi nyumbani, kujilinda, kusitishwa kwa shughuli za kawaida, kudhibitiwa kwa kutoka sehemu moja hadi nyingine, ilani za kukaa nyumbani, kusimamishwa biashara, maduka na huduma kufungwa au kufunguliwa kwa muda maalum tu. Matokeo yake ni kwamba maisha ya kawaida yametatizika na hali ya kutokuwepo usawa imeongezeka na kutiwa chumvi kati ya jamii na ndani ya jamii jambo ambalo limeathiri upatikanaji wa chakula, nyumba, ajira, afya na huduma nyingine za jamii. Haki hizi muhimu pamoja na nyinginezo zimedorora, haswa kwa wale walio hatarini katika jamii zetu.

Kwa habari zaidi kuhusu COVID-19 tafadhali tazama anglicanalliance.org/COVID-19-kuujua ukweli "***Knowing the Facts***" section of the COVID-19 resource hub.

Ulimwengu usio na usawa

Katika maandiko, simulizi ya Mungu na mwanadamu ni simulizi ya mahusiano na kutamani mahusiano: Mungu anatafuta kwa gharama kubwa kuwa na uhusiano nasi; kutafuta kwetu kuwa na uhusiano na Mungu; na uhusiano wa sisi kwa sisi.

Mahusiano ni muhimu katika kunawiri kwa mwanadamu– maisha ye utele ambayo Mungu anawatakia watoto wake wote. Hata hivyo, katika makanisa yetu na katika jamii ulimwenguni kote tunapungukiwa na mambo hayo. Jinsi tunavyochukuliana, mitazamo yetu, dhana zisizothibitishwa, ubaguzi, chuki isiyokuwa na sababu, na matarajio, haya yote yanaweza kuleta dhuluma na kuwapakaza mzigo usiokuwa wa haki wale walio hatarini katika jamii zetu.

Nguvu zisizokuwa sawa na ubaguzi kati ya wanawake na wanaume, iwe miongoni mwa watu binafsi au karibu nasi katika jimii zetu, utamaduni, makanisa na sheria, huleta uharibifu mkubwa. Wanawake na wasichana, wanaume na wavulana huenda wakashawishiwa kwa mitazamo ya kitamaduni na kutoyaelewa maandiko vizuri, hali hiyo inaweza kuwafanya wawatawale wengine na kuwadhulumu. Wanawake na wasichana mara kwa mara huathiriwana matokeo mabaya ya ukosefu wa usawa katika jamii zetu.

Dhuluma za kijinsia ndizo chanzo na matokeo ya uhusiano usiokuwa wa nguvu sawa baina ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana. Mara kwa mara dhuluma hizi huzidi wakati wa majanga ya kimataifa, vita na ghasia za kisiasa wakati itikadi za ukosefu wa usawa zinapodhirishwa na kutumiwa kuendekeza matumizi mabaya ya mamlaka na utawala dhidi ya mtu mwingine.

Je, Biblia inasema nini kuhusu dhuluma?

Mungu ni Mungu wa upendo na anawaita wanadamu wote waishi katika mahusiano ya kupendana. Hata hivyo unyanyasaji na dhuluma bado vipo katika jamii zetu na Bibia inatambua hili na inaakisi uzoefu wetu katika maisha. Cha kusikitisha ni kwamba unyanyasaji na dhuluma zinaweza kumwathiri mtu yeyote wakati wowote. Unyanyasaji na dhuluma humdunisha mtu na zinaweza kumsambaratisha, na kumzuia asiweze kunawiri kikamilifu na kuwa vile Mungu alivyomuumbia awe. Madhara yake yanaweza kudumu maisha yote.

Mungu hajayatupia kisogo haya masuala magumu. Katika 2 Samueli 13 tunasoma kuhusu kubakwa kwa Tamari, binti mfalme na binti yake Mfalme Daudi, alibakwa na ndugu yake Amnoni. Matokeo ya unyanyasafi aliofanyiwa Tamari yalikuwa makubwa sana kiasi kwamba aliishi kama mwanamke mkiwa baada ya kubakwa. Yesu anachukia unyanyasaji na dhuluma na madhara yake kwa mwathriwa. ***Ni dhambi***.

Malaki 2:14 inatuambia kwamba Mungu anaona jinsi mke anavyotendewa na mume wake, 'Ni kwa sababu BWANA amekuwa shahidi kati ya wewe na mke wa ujana wako, ULIYEMTENDA MAMBO YA HIANA, ingawa YEYE NI MWENZAKO, na mke wa agano lako.' Bwana anaona ndani ya nyumba zilizofungwa milango na anajua dhuluma ipo. Malaki 2:14 pia inatukumbusha kuhusu viapo na agano la ndoa mbele za Mungu kwamba tutapendana na kutunzana. Katika Zaburi 11:5 tunasoma ujumbe wa wazi na mzito unaopinga dhuluma, 'BWANA humjaribu mwenye haki; Bali nafsi yake humchukia asiye haki, Na mwenye kupenda udhalimu.'

Yesu ndiye mfano tunaofuata sisi Wakristo. Maisha ya Yesu duniani yalituonesha jinsi ya kuishi na kutendeana. Yesu anaufunua udhalimu, analeta uponyaji na anakabiliana na watu wenye mamlaka wakati wanakosa kuwatendea watu haki. Katika Yohana 8:2-11 tunaona jinsi Yesu alivyoyalinda maisha ya mwanamke aliyefumaniwa akizini na alikuwa karibu kupigwa mawe na watu. Aliongea na mwanamke pale kisimani ambaye alikuwa na waume watano na akamwonesha heshima na hadhi (Yohana 4). Wakolosai 3:19 inaongea wazi katika maagizo yake, 'Ninyi waume, wapendeni wake zenu msiwe na uchungu nao.' Waefeso 5:29 inasema wazi maana ya hayo katika matendo: 'Maana hakuna mtu anayeuchukia mwili wake po pote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa'. Wakati dhuluma inapotokea wale walionusurika wanaweza kuhakikishwa kwamba kutafuta pa kukimbilia kutokana na dhuluma ni jambo la busara kutenda ili kujiepusha na madhara (Zaburi 22:3).

Wakristo wameitwa kuishi maisha ya upendo, na kuwa mfano wa mahusiano bora yenye upendo, ili kumwezesha kila mtu anawiri katika kile alichotuumbia Mungu. 1 Wakorintho 13:4-7 inatuambia: Upendo huvumilia, hufadhili. upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni. haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya, haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli, huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote.

Ni wazi kwamba Mungu anataka tuwapende watu, wala si kuwatumia na kuwadhulumu, wengine. Katika maandiko hakuna haki yoyote au kijisababu cha kuendekeza dhuluma za kinyumbani na dhuluma za kijinsia.

Dhuluma za nyumbani ni nini?

Dhuluma za nyumbani ni tukio lolote au msururu wa matukio ya kutawala, tabia ya kuonea au kutisha, unyanyasaji au dhuluma. Hata ingawa dhuluma zinaweza kutokea katika umri wowote, makala haya yanaangazia watu wazima wa kike ambao wako katika mahusiano au wamekuwa katika mahusiano na watu wengine. Hii inajumuisha dhuluma za kimwili, kingono, kiasaikolojia, kihisia, za maneno na za kifedha.

Hata hivyo, tunahitaji kuwa macho kutambua unyanyasaji na dhuluma za kingono kwa wasichana waliovunja ungo* na hata wadogo zaidi hususan katika wakati wa janga ambapo kiwango chao cha kuwa hatarini huongezeka. Kw mfano, ndoa za mapema na/au za lazima, mimba, ukahaba unaotokana na umaskini na ubakaji, huongezeka sana wakati wa majanga ya kimataifa na wakati wa migogoro.

Tabia ya kuwatawala watu ni matendo kadhaa ambayo lengo lake ni kumfanya mtu kuwa chini na/au amtegemee yule anayemdhuluma kwa kutumia mbinu nyingi mbalimbali, zikijumuisha kumzuia kuwasiliana na familia yake, marafiki na jamii ili kuleta hali ya upweke tegemezi. Tabia ya kuonea watu ni tendo au msururu wa matendo ya uvamizi, vitisho, kuaibisha na kudunisha au dhuluma nyingine zinazotumiwa kudhuru, kuadhibu, au kumtisha mwathiriwa.

Kiini haswa cha dhuluma za nyumbani ni utumizi mbaya wa mamlaka na kumtawala mtu mwingine. Ni kule kumtumia mtu mwingine kwa njia yoyote ile kumlazimisha afanye kile unachotaka afanye pasipo kujali kamwe utunzaji wake, maslahi, maisha au uhuru wake. Hiyo ni dhambi. Hali hii inatokana na imani ya mdhulumu kwamba ana haki na fursa ya kufanya hivyo, kwamba yule mwanamke yuko chini na yupo kwa ajili ya kutimiza matakwa ya mdhulumu. Katika nchi nyingi ni hilo ni kosa la jinai na hivyo tendo hilo linafaa kuonekana hivyo.

Tambua itikadi za uwongo kuhusu dhuluma, kama vile, 'alifanya hivyo kwa sababu alikuwa amekasirika', au alikuwa anakunywa pombe, au alikuwa ametumia dawa za kulevya, au ana matatizo ya kiakili. Hivi huenda ni vipengele vinavyochangia dhuluma lakini sivyo vinavyosababisha dhuluma. Mtekelezaji wa dhuluma huamua kudhulumu. Ni uamuzi anaoufanya kwa hiari yake mwenyewe.

Dhuluma za nyumbani ni tofauti na mahusiano ambapo tabia zisizofaa hutokea (kama vile watu kufokeana miongoni mwa watu wawili katika hali ambazo kuna mvutano). Hata hivyo, pale ambapo kuna tabia zisizofaa, hatari za kutokea hali ya dhuluma huongezeka, kwa kuwa mtu mmoja hutaka kumtawala mwenziwe katika uhusiano wao. Kwa mfano, mahusiano yasiyokuwa mazuri yanaweza kugeuka na kuwa dhuluma za nyumbani wakati kuna nia ya kushinda mabishano kwa vyovyote vile, kumshinda mtu mwingine na kumfanya ahisi vibaya, na kufanya mambo yaende utakavyo pasipo kuwajali wengine walio katika nyumba hiyo.

** Shirika la Afya Duniani (WHO) linamwelezea kijana aliyevunja ungo kuwa wale watu wa umri wa kati ya miaka 10 hadi 19. Kwa hiyo vijana wengi waliovunja ungo, wamejumuishwa katika ufafanuzi unaotegemea umri wa "mtoto", kama ilivyonukuliwa na kubadilishwa na Convention on the Rights of the Child,4 kama mtu aliye chini ya miaka 18.*

Je, dhuluma za nyumbani ni suala zito kiasi gani?

Mmoja kati ya wanawake watatu ulimwenguni kote amepitia dhuluma ya kimwili na/au dhuluma ya kingono kutoka kwa mpenzi wake wa karibu. Kiwanga hiko hupanda hadi asilimia 70 katika baadhi ya nchi.

Dhuluma za nyumbani pia huwakumba watu wanaokwenda kanisani, mara kwa mara wakiwa kama kioo cha yale yanayoendelea katika jamii zetu. Ni suala zito ambalo linaweza kusababisha kifo. Shirika la UN Women linasema kwamba kwa siku takriban wanawake 82 huuawa kwa makusudi na wapenzi wao wa sasa au wa zamani. Aina zote za unyanyasafi, zikiwemo za kijinsia, kingono na unyanyasaji kutoka kwa wapenzi, huenda zikazidisha uwezekano wa mwanamke kuambukizwa virusi vya UKIMWI na aina nyinginezo za magonjwa ya zinaa. Wanawake wachanga na wasichana waliovunja ungo ndio walio na uwezekano mkubwa zaidi wa kudhulumiwa na wapenzi wao; katika mazingira mengine, asilimia 45 ya wasichana waliovunja ungo wanasema kwamba tendo lao la kwanza la ngono lilikuwa la kulazimishwa. Wanawake wachanga wanaodhulumiwa na wapenzi wao wana uwezekano wa asilimia 50 wa kuambukizwa virusi vya UKIMWI kuliko wanawake wengine (UNAIDS 2015c, 37).

Kumekuwa na ongezeko katika unyanyasafi wa jinsia wa ndani na wa umma katika kipindi cha COVID-19. Baadhi ya nchi zimeshuhudia dhuluma za nyumbani zikiongezeka kwa thuluthi moja. Angalia takwimu za nchi yako za kiwango cha dhuluma za nyumbani na ongezeko lolote katika kipindi cha COVID-19 (pia tazama Kiambatanisho 2). Dhuluma za nyumbani ni suala la jinsia na hiyo inamaanisha kwamba litawaathiri kwa kiasi kikubwa wanawake kuliko wanaume. Hiyo inamaanisha kwamba baadhi ya wanaume pia watakuwa waathiriwa na manusura wa dhuluma za nyumbani. Dhuluma zote ni makosa na lazima zikome na manusura yeyote anahitaji kusaidiwa na kushikwa mkono ili apone na kurudi katika hali yake.

Je, athari za COVID-19 katika dhuluma za nyumbani ni zipi?

Nchi nyingi zimeshuhudia ongezeko la dhuluma za nyumbani na simu zinazopigwa kwenye nambari za kitaifa za usaidizi wakati wa kipindi cha kusitishwa kwa shughuli za kawaida na ilani za kukaa nyumbani kutokana na COVID-19.

Kwa mfano, Afrika Kusini walipokea simu 87,000 kupitia nambari ya usaidizi wa dhuluma za nyumbani katika mwezi wa kwanza wa lockdown, na Malaysia walishuhudia ongezeko la 44% la simu zinazopigwa kwenye nambari ya usaidizi. Nchini Kenya kuna msichana wa miaka 16 ambaye alitekwa na mwanaume na kudhulumiwa kingono. Yule mtekaji alisema kwamba alimteka kwa sababu alihitaji mtu wa kuwa naye katika muda wa kusitishwa kwa shughuli za kawaida na serikali kwa sababu ya COVID-19 (Human Rights Watch, April 2020).

Kujitenga ni mbinu kuu kwa mdhulumu, imerahisishwa na ilani ya serikali ya watu kukaa nyumbani wakati wa COVID-19 na ambapo hakuna njia yoyote ya kuwawewezesha manusura wa dhuluma kutoroka. Mdhulumu/mnyanyasaji anaweza kutawala karibu kila hali ya maisha ya mwanamke wakati akiwa kwenye lockdown ili asiweze kuishi akiwa huru. Huenda asiweze kwenda madukani kununua chakula kwa sababu serikali iliweka mipaka, au kwa sababu yule mwanamume wake anatawala pesa zote na hampi pesa anazohitaji kununua mahitaji kama vile chakula, sabuni na vitu vingine vya usafi vya kudumisha afya, kumfanya msafi na katika hali nzuri (hali hii inajulikana kama dhuluma ya kifedha). Mnyanyasaji anaweza kumlazimisha kufanya ngono kinyume na mapenzi yake (kumbaka) au anaweza kutumia maandiko vibaya kumshurutisha manusura kufanya naye mapenzi. Yule manusura pasipo kuwa na pa kutorokea, huenda akahisi hana la kufanya isipokuwa kumliwaza mnyanyasaji (hii ni dhuluma ya ngono). Agizo la serikali la watu kukaa nyumbani linaweza kuifanya mikakati ya wanawake kujitetea na kuwakatalia wanyanyasaji kuwa na mipaka, kupungua, au kukosa maana yoyote.

Ni muhimu kwamba kila mtu afahamu maagizo ya serikali na ya kisheria yanasema nini ili kusiwe na hali ya kuchanganyikiwa kuhusu maagizo ya lazima au yale yanayoruhusiwa. Kwa mfano, katika nchi nyingine, maagizo ya kukaa nyumbani yanaweza kukiukwa katika mazingira ya dhuluma za nyumbani ili manusura aweze kupata msaada anaohitaji.



Hatua wanazopaswa kuchukua viongozi wa makanisa na majirani wema

Usalama wa mwathiriwa/manusura na watoto wake ndicho kitu kinachofaa kupewa kipau mbele wakati wote. Kuhakikisha manusura na watoto wake wako salama ni agizo. Hakikisha hatua unayochukua inakufanya uwe salama pia.

Unaposhughulikia dhuluma za nyumbani, ni vyema kutumia TIMA kama kumbukumbu ya huo mchakato. Haya ni Tambua, Itikia, Mtume na Andika. Hata katika mazingira ya lockdown (kusitishwa kwa shughuli za kawaida) au maagizo ya kutokaribiana na watu, kanuni hizi zinaweza kutumika.

1. **Tambua** kwamba dhuluma za nyumbani pia hutokea katika jamii za makanisa na yamkini kiwango chake kitaongezeka na kuenea katika kipindi cha COVID-19. Jifunze kutambua dalili za dhuluma (angalia chati hapa chini) na uwe tayari kuchukua hatua ifaavyo kwa kuzingatia maagizo yaliyowekwa (kutokaribiana n.k.)
2. **Itikia** kwa kusema naamini yale unayosema. Haya yanaweza kufanyika kupitia mtandao, kupitia ujumbe mfupi au WhatsApp na vile vile ana kwa ana wakati lockdown (kusitishwa kwa shughuli za kawaida) kutakapokwisha. Manusura wengi watakuwa wameambiwa au wanahisi hakuna mtu atakayewaamini na kwamba hakuna mtu atakayewasaidia. Kuwasaidia kuandaa mpango wa usalaa ni hatua nzuri ya kuchukua (tazama chati hapa chini).
3. **Mtume** manusura kwa huduma za eneo au za kitaifa zinazotolewa waathiriwa wa dhuluma za nyumbani, ikiwa zinapatikana katika nchi yako (kinganishi cha habari hizi kiko katika chati hapa chini). Ikiwa maisha ya manusura yako hatarini wakati huo, basi wapigie polisi kwa kutumia namba ya dharura. Dhuluma za nyumbani zinaweza kutishia maisha ya mtu na zinahitaji kuchukuliwa kwa uzito. Tazama chati uone hatua nginginezo.
4. **Andika** yale manusura amesema. Hizi zinaweza kuwa kumbukumbu au picha za ushahidi wa kitu kinachoweza kuonekana. Wakati wote mwombe manusura ruhusa kabla hujapiga picha.

Hata katika wakati wa janga hili la kimataifa kuna hatua za kiutendaji tunazoweza kuchukua.

Nani/Nini	Jukumu la Majirani Wema	Jukumu la Viongozi wa Kanisa
Tambua dalili za dhuluma za nyumbani	Tafuta dalili za dhuluma kama vile: 1. mwanamke wakati wote hayuko peke yake, anaonekana mwenye huzuni na anasikitisha, 2. hawezi kujilisha mwenyewe au watoto wake, 3. ana majeraha yasiyojulikana chanzo chake, 4. anaonekana kuugua mara kwa mara, 5. mpenzi wake anasema yeye ni mjinga, hana maana, na hawezi kufanya chochote. 6. Mpenzi wake anamtusi na kumkosoa. • Tambua kwamba kile unachokiona na kukisikia mwanzoni yamkini ni kionjo tu cha hiyo dhuluma. • Andika kauli fulani kwenye mtandao wa kijamii kusema kwamba unafahamu kuhusu dhuluma za nyumbani na kwamba uko salama kuzizungumzia. • Tambua hatari haswa iliyopo kwa wasichana waliovunja ungo na wasichana kwa jumla, hatari ya kunyanyaswa kingono na kudhulumiwa, hususan wakati wamemaliza shule. • Jihadhari na wanaume wanaotoa vitu hivi vinne: pesa, nguo, simu na lifti kwa wasichana wachanga. Hili huchochea unyanyasi na dhuluma siku zijazo. • Tambua wasichana waliovunja ungo wakiwa nyumbani peke yao na jamaa zao wanaweza kudhulumiwa. • Tambua kwamba watoto wakiwa nyumbani wanashuhudia kinachoendelea na wao wenyewe wanaweza kudhulumiwa. Watoto wanaweza kutumiwa kama chombo cha kumdhulumu mwanamke.	Tafuta dalili za dhuluma kama vile: • mwanamke haruhusiwi kuhudhuria ibada kwenye mtandao, kuomba au kusoma Biblia. • ana majeraha yasiyojulikana chanzo chake au anaonekana kuugua mara kwa mara. • mpenzi wake anamkosoa, na kuongea maneno mabaya juu yake na hamheshimu. • Mnyanyasaji/mdhulumu anaweza kusema kuwa mpenzi wake wakati wote analalamika na anampa wakati mgumu. Kuwa na busara kuhusu kulazimishwa na mnyanyasaji kuitetea dhuluma. Wanyanyasaji wanaweza kuwa wachangamfu na mara kwa mara hujaribu kujitafutia uungwaji mkono kwa kuwasaidia watu wa nje kwa kuwa hili huyafanya maneno ya mwanamke yasiaminiwe. Tambua hatari haswa iliyopo kwa wasichana waliovunja ungo na wasichana kwa jumla, hatari ya kunyanyaswa kingono na kudhulumiwa wakati wamemaliza shule. Kuwa mwenye busara kwa wanaume wanaotoa vitu hivi vinne: pesa, nguo, simu na lifti kwa wasichana wachanga. Hili huchochea unyanyasi na dhuluma siku zijazo. Tambua kwamba watoto wakiwa nyumbani kuna uwezekano wa kushuhudia kinachoendelea na wao wenyewe wanaweza kudhulumiwa. Watoto wanaweza kutumiwa kama chombo cha kumdhulumia mwanamke. Tambua wasichana waliovunja ungo wakiwa nyumbani peke yao na jamaa zao wanaweza kudhulumiwa.

Nani/Nini	Jukumu la Majirani Wema	Jukumu la Viongozi wa Kanisa
Itikia	• Sema ninayaamini maneno yako maana kutakuwa na woga mwingi kwamba hakuna mtu ataamini dhuluma imekuwa ikiendelea. • Sikiliza kwa makini kile anachosema. Mwambie hayo si makosa yake na kwamba ana haki ya kuzungumzia suala hilo na kuomba msaada. • Tafuta ni njia gani salama ya kuwasiliana naye, ujumbe mfupi, WhatsApp, au simu. • Pendekeza kwamba aandae mpango wa usalama wa ndani ya nyumba (vyumba vyenye kufuli mlangoni, chembeo za mlango n.k.) na mpango wa kutoka kwa usalama, ikiwa ataamua anahitaji kuondoka kwa usalama wake mwenyewe na kwa usalama wa watoto. • Unda neno la siri la kutumia na manusura, kama vile jina linaloanza na A, ili ujue wakati yuko katika hatari kubwa ya dhuluma. • Pendekeza ahamie kwa rafiki au nyumbani kwa jamaa wa familia, mama, dada au shangazi ambao wana huruma na wanaelewa unyanyasaji wa nyumbani au wamefundishwa kushughulikia hali hizi. Usalama ndilo jambo la kupewa kipau mbele. Nchi nyingi zinaruhusu mtu kutoka nyumbani endapo atakuwa ni manusura anayetoroka kudhulumiwa. • Toa viunganishi vya usafiri unaopatikana. Nchi nyingine zinatoa usafiri wa bure kwa manusura wanaokimbia dhuluma kama vile tikiti ya bure ya treni ya kutorokea mahali au teksi ya kwenda mahali salama. • Je, kuna mfuko wa dharura unaoweza kupatikana kama vile mfuko wa kitaifa/ halmashauri au • mfuko wa dharura wa kanisa au wa kikundi cha kujisaidia? Hii inaweza kutoa mfuko wa awali wa kumwezesha kupata mahali salama au kufika katika eneo salama. • Je, kuna vocha za chakula zinazopatikana kutoka kanisani au kituo cha jamii cha mtaa ili manusura aweze kujilisha yeye mwenyewe na watoto?	• Wasikilize na uyaamini maneno ya manusura wa dhuluma na uwaambie kwamba kudhulumiwa kwao si makosa yao na kwamba wanafanya jambo sahihi kufichua dhuluma hizo. • Tafuta ni njia gani salama ya kuwasiliana naye, ujumbe mfupi, WhatsApp, au simu. • Unda neno la siri ili uweze kujua anapokuwa hatarini zaidi ya kudhulumiwa zaidi. • Je, kuna mfuko wa dharura wa kanisa unaoweza kusaidia manusura kupata usafiri kwenda nyumbani kwa jamaa yake apate usalama, au kwenda kwa jamaa yake aliye katika mkoa ulio karibu? Ikiwa ndiyo, toa pesa za dharura na mwongozo juu ya usafiri unaopatikana. Fedha zinaweza kupewa yule manusura aondoke na aweze kufika kwenye makazi ya dharura kwa siku chache au wiki. • Usalama daima ni jambo la kupewa kipaumbele na fedha zinaweza kuwa kizuizi kikubwa cha kupata msaada na kushikwa mkono. • Je, kuna vocha za chakula ambazo kanisa linaweza kutoa ili manusura aweze kujilisha yeye mwenyewe na watoto? • Ikiwa hakuna nyumba salama au mahali pa kukimbila, toa kanisa liwe kimbilio kwa waliodhulumiwa. Hii inaweza kuwa hatari, na katika nchi zingine kuwa haramu, kwa hivyo inahitaji uangalifu mkubwa ikiwa kanisa litatumiwa kama kimbilio. • Pakua nakala ya Restored Church Pack on ending Domestic Abuse ili upate habari na mawazo zaidi. Yanapatikana katika • lugha mbalimbali. Kiunganishi kinapatikana pia kwenye viambatanisho. • Jumuisha mada ya dhuluma za nyumbani katika mahubiri yako, sala, liturujia na matangazo wakati wa ibada ili kuhakikisha kuwa washirika wako wanajua dhuluma za nyumbani ni nini na kwamba msaada unapatikana. • Sema kwamba dhuluma za nyumbani ni dhambi, ni makosa, na hazikubaliki kamwe na lazima zisitishwe. Jumbe za wazi kutoka kwa kiongozi wa kanisa zinaweza kusaidia kuzuia wanyanyasaji kutotetea dhuluma zao ndani ya nyumba. • Bandika mabango ndani ya kanisa lako au nje ya kanisa lako kuhusu dhuluma za nyumbani na watoa huduma wa dhuluma za nyumbani ili watu wanaopita wayaone. • Weka matangazo kwenye wavuti yako ya kanisa na kurasa za Facebook kuhusu dhuluma za nyumbani na wapi kwa kupata msaada na kushikwa mkono. • Tuma barua kwa wachungaji na viongozi wa kanisa wafahamu kuongezeka • kwa uwezekano wa kutokea dhuluma za nyumbani na uwatie moyo kuzungumza juu yake katika mahubiri/ matangazo ya kanisa na vibao vya matangazo na kwenye mitandao ya kijamii.

Nani/Nini	Jukumu la Majirani Wema	Jukumu la Viongozi wa Kanisa
Mtume	• Toa maelezo ya huduma za dhuluma za nyumbani ikiwa kuna zozote hapo ulipo. Ikiwa hakuna, mpe namba ya kitaifa ya huduma hizo. Tazama Hot Peach Pages www.hotpeachpages.net/ upate orodha ya nambari za simu za nchi zote katika lugha mbalimbali. • Ikiwa unyanyasaji na dhuluma zinatishia maisha mhimize manusura awapigie simu polisi. • Mara kwa mara manusura wanaweza kutolipatia uzito suala la dhuluma zinazotokea na wakakosa kuelewa uzito wa hali waliyomo. Ikiwa wanakataa kupata msaada, lakini kuna watoto walio hatarini nyumbani, utahitaji kufuata mwongozo wa ulinzi wa watoto na upige ripoti kwa huduma za kijamii, au polisi ikiwa huduma za kijamii hazipo. • Ikiwa kuna Muungano wa Akina Mama, muunganishe manusura kwenye mtandao huo ili akae na watu, apate msaada na ashikwe mkono ikiwa inafaa.	• Toa maelezo ya huduma za dhuluma za nyumbani za eneo hilo au za kitaifa ikiwa zipo. Tazama https://www.hotpeachpages.net/ upate nambari za simu za kitaifa za kuitisha msaada duniani kote. • Ikiwa hakuna huduma za dhuluma za nyumbani sasa au haziwezi kufikiwa, wasiliana na afisa wa usalama, afisa wa ulinzi wa watoto, mchungaji wa kanisani kwako au kiongozi wa kike kwa msaada zaidi na ushikwaji mkono. • Rejelea Bibilia na ueleze kwamba Mungu anachukia dhuluma na unyanyasaji na uwahakikishe kuwa ni sawa kufichua dhuluma. • Muunganishe manusura katika Muungano wa Akina Mama kwa msaada na akae nao haswa ikiwa hakuna watoa huduma wa dhuluma za nyumbani katika eneo hilo. • Pakua nakala ya Restored Church Pack on ending Domestic Abuse ili upate habari na mawazo zaidi.
Andika	• Andika kumbukumbu nzuri ya yale yaliyosemwa. Andika haraka iwezekanavyo yale yaliyosemwa mara tu manusura anapofichua. Usiandike maoni yako mwenyewe lakini andika tu yale ambayo umesikia. Andika tarehe, saa za matukio endapo umeambiwa. Andika kwa kifupi tarehe na wakati wa habari kufichuliwa. • Weka kumbukumbu hiyo mahali salama. Inaweza kutumiwa baadaye na polisi au kortini kama ushahidi. • Weka kumbukumbu ya msaada wako mwenyewe na ushauri uliompa manusura wa dhuluma, kwa mfano unaweza kuandika kwamba ulimpa kijikaratasi au nambari ya simu ya huduma za dhuluma za nyumbani, au kwamba ulielezea alikuwa katika hatari kwa kiasi gani.	• Weka kumbukumbu sahihi ya habari zote zilizofichuliwa siku ile zilipofichuliwa. Ni muhimu kuandika maneno ya manusura na sio maoni yako mwenyewe juu ya suala hilo. • Weka kumbukumbu hiyo mahali salama na usimfichulie mtu yeyote isipokuwa 'Afisa wa Ulinzi' au Afisa wa Ulinzi wa Watoto au Mchungaji ikiwa una mmoja kanisani. • Weka kumbukumbu ya msaada wako mwenyewe na ushauri uliompa manusura wa dhuluma, kwa mfano unaweza kuandika kwamba ulimpa kijikaratasi au nambari ya simu ya huduma za dhuluma za nyumbani, au kwamba ulielezea alikuwa katika hatari kwa kiasi gani.

** Hili ni jukumu muhimu na linapaswa kuzingatiwa tu wakati hakuna njia nyingine inayopatikana kamwe. Milango ya kanisa inahitaji kufungwa na ufunguo mmoja uweze kupewa manusura na mwingine upewe mtu mwingine pekee. Mnyanyasaji/mdhulumu lazima asijue mahali alipo manusura. Inaweza kuwa hatari. Chunguza ikiwa hii ni shughuli halali ndani ya nchi yako kabla ya kuwaza kuchukua hatua hii.

Please note the image above is a licensed stock photo, intended for illustrative purposes only and all persons depicted are models.

Kile kisichofaa kufanya

USIMUULIZE MNYANYASAJI IKIWA KILE ANACHOSEMA MANUSURA NI KWELI KWA KUWA HILI LINAWEZA KUMWEKA MWATHIRIWA KATIKA HATARI YA KUDHURIWA ZAIDI NA LINAWEZA KUSABABISHA KIFO.

Ni muhimu wakati Manusura anapofichua dhuluma kwamba hatuipunguzi dhuluma makali, kuitolea sababu, kuona ni haki au kuifanya kuwa ya kiroho. Usiombe ushahidi, usimlaumu au kumuomba arudi kwa mumewe au mpenzi wake kwani inaweza kuwa si salama kufanya hivyo. Usiweke ahadi zisizokuwa za kweli. Utambue uwezo na rasilimali zako.

Usiwatume wapenzi hao kwenda kupokea ushauri nasaha au upatanisho kwa kuwa kufanya hivyo inaweka sehemu ya lawama kwa manusura na kumwondolea lawama kiasi mnyanyasajii ambaye anafaa kulaumiwa kikamilifu kwa matendo yake na matokeo ya matendo yake.

Hatua Anazoweza Kuchukua Manusura

Manusura pia wana uwezo na wanaweza kuchukua hatua zifuatazo, kulingana na hali zao.

Kile manusura anaweza kufanya	Jinsi hili linavyoonekana ki matendo
Tambua kwamba unadhulumiwa	Kupiga kelele, kulaumu, kukupiga, kutokuruhusu utoke nje, kukuzuia kuongea na wengine, kukupokonya pesa au kukupimia pesa ni mifano ya dhuluma za nyumbani.
Itikia kwa kutafuta msaada na uhakikishe uko salama	• Wapigie simu polisi unapokuwa katika hatari. • Piga simu kwa kutumia nambari za simu zinazohusiana na dhuluma katika nchi yako au eneo lako endapo zipo. • Omba usaidizi. Dhuluma iliyotokea sio makosa yako, haijalishi ni mara ngapi mnyanyasaji anakuambia kwamba ulimfanya akudhulumu. • Hakikisha uko salama nyumbani kwako na andaa mpango wa usalama. Mwachie jirani mwema unayemwamini nguo zako za ziada, stakabadhi muhimu za kibinafsi na kicha cha funguo. • Unda neno la siri kwa ajili ya jirani yako, kiongozi wa kanisa au mwajiri wako ili aweze kujua wakati unahitaji msaada. Kwa mfano, ukianza kuzungumza juu ya Angela, au jina lingine linaloanza na A ambalo mmekubaliana, katika mazungumzo yenu mtu huyo mwingine atajua kuwa uko hatarini na unahitaji msaada. • Kuwa mwangalifu na wanaume wanaojitolea kukuokoa na kukupa nyumba ukae pamoja nao wakati huu wa hatari. Hii mara kwa mara husababisha unyanyasaji zaidi na dhuluma katika siku zijazo.
Mtume/Jitume mwenyewe kwenye huduma za dhuluma za nyumbani zinazopatikana.	• Pigia simu huduma za dhuluma za nyumbani. Hifadhi nambari katika simu yako kwa kutumia jina la kike linaloanza na A, kama vile Angela, ili iweze kuwa ya kwanza kwenye orodha ya namba ulizo nazo. • Ikiwa polisi wamepigiwa simu weka kumbukumbu ya nambari ya uhalifu kwa ajili ya ufuatiliaji. Omba upigiwe simu tena ama utembelewe ikiwa hili linawezekana. • Ikiwa hakuna huduma za dhuluma za nyumbani zinazopatikana katika eneo lako wasiliana na mtu wako wa Muungano wa Akina Mama akuunganishe na mtandao ili ushikwe mkono na upate msaada. Hauko peke yako katika haya.
Andika matukio yoyote ya dhuluma kwa marejeleo ya baadaye	• Ikiwezekana na pasipo mnyanyasaji kujua, andika kumbukumbu yenye tarehe, saa na kile kilichotokea kwako. Mambo haya yanaweza kutumiwa kama ushahidi baadaye endapo itakulazimu kuyapeleka mbele. • Piga picha na uzihifadhi kwenye faili ya jumla katika simu yako kama vile kutumia jina majirani. • Mwombe jirani yako/kiongozi wa kanisa/mwajiri kuweka kumbukumbu ikiwa atasikia au ataona udhuluma ikitokea na pia unapowafichulia dhuluma hiyo. Kumbukumbu hizi zinaweza kutumika baadaye kortini endapo zitahitajika.

Kuwashirikisha Wanaume

Ikiwa tunataka kuona mwisho wa dhuluma za nyumbani, basi kuwashirikisha wanaume katika hatua zitakazochukuliwa ni muhimu katika kuleta mabadiliko kamili yanayohitajika. Wanaume wanaweza kuwa mfano mwema wa uanaume na kukabiliana na mitazamo na matendo ya wanaume wengine yanayodunisha, yanayoshusha na kuwaangamiza wengine.



Ni muhimu sana kwamba wanaume waishi maisha ya kufuata mfano wa Yesu na kuchukua msimamo kuhusu dhuluma za nyumbani. Kuonesha mfano mzuri, mahusiano mazuri ni muhimu katika kudumisha nyumba nzuri na iliyokamilika. Vile vile ni ushuhuda mzuri sana kwa majirani zako na unawapa manusura wa dhuluma mfano wa jinsi maisha yanavyoweza kuwa pasipo dhuluma.

Kuchangamana kwa wanaume na watu wengine katika tamaduni nyingi na ulimwenguni kote, hutoa mtazamo mbaya wa uanaume ambao unaweza kuwa sumu. Hili linaweza kusababisha kukua kwa mitazamo inayodhuru ambayo inaweza kuwaharibu wanaume na wanawake walio katika mahusiano. Matarajio ya kijamii yaliyowekwa kwa wanaume ambayo si ya kweli na ni finyu yanaweza kujitokeza wakati wamesimamishwa kazi, na wanaume ambao hawafanyi kazi wanaweza kukosa ujuzi (kama vile kupika) wanapojizoesha mazingira mapya. Wanaume huenda watahitaji kutafakari juu ya mitazamo ambayo wamekuzwa nayo, na kile wanachopaswa kubadisha ili kuhakikisha wanaendesha nyumba zao kwa njia nzuri, ya ushirikiano na yenye matokeo bora. Huu ndio wakati wa misingi mipya kujengwa kwa ajili ya siku zijazo baada ya COVID-19.

Kutokana na mseto wa mtindo wa maisha mahali pamoja kama vile kufanyia kazi nyumbani na watoto kusomea nyumbani, kusimamia nyumba vizuri ni muhimu sana katika kuhakikisha maisha yanakwenda vizuri katika kipindi cha lockdown. Hii inamaanisha kuwepo kwa majadiliano ya wazi na ya kweli kuhusu kusimamia nyumba na kugawa majukumu kwa njia ya usawa pasipo kuwaonea wengine. Kuandaa ratiba ya saa 24 za nani atafanya nini kila saa ya siku, kunaweza kuwa mwanzo mzuri katika kupanga kazi zote zinazofanywa, na ni nani anayefanya kazi ipi na kazi hiyo inachukua muda gani. Hii inatoa msingi wa majadiliano katika kugawa upya majukumu ili kusiwe na mtu yeyote katika nyumba anayelemewa na kazi. Hii inaweza kumaanisha kwamba stadi mpya zinahitaji kukuzwa kwa msaada na ushauri kutoka kwa wengine. Ishara nyingine ambayo huenda ikakuonesha ukosefu wa usawa ni kuangalia ni nani amekaa kwenye sofa kwa muda mrefu zaidi au anatazama TV zaidi wakati wengine wanafanya kazi hapo nyumbani. Kile kinachofaa katika nyumba moja kitakuwa tofauti na nyumba nyingine lakini kilicho muhimu ni kutochukulia kwamba fulani 'sharti' afanye jambo fulani kwa misingi ya tamaduni au jinsia.

Swali muhimu la kujiuliza ni hili: **'Je, kile ninachofanya kinaathirije uhusiano wangu na watu wengine?'** Kutafakari huku hutuwezesha kutathmini ikiwa mtazamo wetu, matendo na tabia zetu hufanya tujengane au husababisha kuvunjika kwa uhusiano.

Hatua nzuri ambazo wanaume wanaweza kuzichukua wakati wa agizo la kukaa nyumbani zinaweza kupatikana katika rasilimali ya 'Men in Lockdown' na 'Men under Pressure' (tazama kiambatanisho 1)

Shirika la Umoja wa Mataifa linaendesha kampeini ya *Mwanamume kwa Ajili ya Mwanamke (He for She)* ili kuwahusisha wanaume katika kufanikisha usawa wa kijinsia. Katika kipindi cha COVID-19 wanafanya kampeini iitwayo#HeForSheAtHome wakiangalia jinsi majukumu na kazi zinavyojadiliwa na kutumiwa kwa ajili ya kufanikisha usimamiaji wa nyumba. Habari zaidi na picha za mawazo mazuri zinapatikana kwenye www.instagram.com/heforshe hapa.

Watekelezaji

Watekelezaji wa dhuluma wanahitaji kuwajibikia matendo yao na ukombozi wao.

Kashfa ya injili ni kwamba upendo, neema na msamaha unapatikana kwa wote. ***Kauli hii haifai kutumiwa kama kijisababu cha kumfanya mnyanyasaji asishtakiwe kwa uhalifu wake.*** Mungu ni Mungu wa haki na vile vile wa upendo na msamaha. Matokeo ya matendo ya mtekelezaji hubaki pale pale na yule aliyenyanyaswa anafaa kutendewa haki.

Wahimize watekelezaji wa dhuluma kutafuta kozi itakayowasaidia kubadilisha mtazamo na tabia zao zinazodhuru. Hakikisha watekelezaji wanawajibikia matendo yao kwa kuwa haki ni muhimu kwa uponyaji wa manusura na kurejesha uaminifu katika ubinadamu na inathibitisha kwamba ilikuwa makosa kwa yeye kudhulumiwa.

Watekelezaji wanaweza kutumia **Mfumo wa Waketelezaji wa** TTOMPAP wa tambua, tubu, ondoa, mtume, patana, andika na pitia kuleta, mabadiliko katika maisha yao na kurekebisha yale makosa yaliyotokea. Maana ya TTOMPAP ni tambua, tubu, ondoa, mtume, patana, andika, pitia tena.

Hatua Ambazo Watekelezaji Wanafaa Kuchukua

Watekelezaji wana uwezo na udhibiti wa kibinafsi wa kuweza kubadilisha mtazamo na tabia zao na kuwajibikia matendo yao.

Kile watekelezaji wanaweza kufanya	Jinsi hili linavyoonekana ki matendo
Tambua kwamba unatekeleza dhuluma	• Kupiga kelele, kupiga, kulaumu, kumtumia mtu vibaya, kudhibiti na kumuonea mtu, kumtenga mtu mwingine ni dhuluma. • Dhuluma hizo ni makosa na lazima zikome • Dhuluma ni jambo unalochagua kulifanya • Dhuluma huleta uchungu mwingi, kiwewe kinachodumu maisha yote, huvunja uaminifu kabisa, • Dhuluma ni dhambi na ni chukizo kwa Mungu, • Dhuluma ni kosa la jinai katika nchi nyingine, • Kubali jinsi ulivyochagua kutekeleza dhuluma na matumizi mabaya ya nguvu na utawala
Tubu	• Makosa uliyofanya • Tambua uzito wa tabia yako na athari za matendo yako kwa wale walio karibu nawe, mpenzi wako, watoto, majirani, jamaa, washirika wa kanisa na jamii. • Ungama dhambi yako kwa Mungu kwa moyo wako wote huku ukikumbuka kwamba Mungu anaona ndani ya mioyo yetu na hadanganywi na maungamo ya uwongo. • Jitoe mhanga kuyabadilisha maisha yako, kuwa tayari kulaumiwa kutokana na matendo yako na mtu ambaye hatashawishiwa na vijisababu vyako. Ungama kwa kiongozi wa kanisa na kwa yule mtu ambaye atahakikisha unawajibikia yale yote uliyotenda. Mungu anasamehe lakini matokeo ya matendo yako hubaki na yanafaa kushughulikiwa.
Ondoa	• Jiondoe katika mazingira na nyumbani ikiwa utakuwa hatari kwa wengine kwa kuendekeza dhuluma zaidi au ikiwa utaombwa kufanya hivyo na mwathiriwa. • Ikiwa mpenzi wako hataki mpatane, lazima uheshimu msimamo wake na ujitahidi uwezavyo kuhakikisha kwamba kujitenga huko ni salama na kwa heshima.
Mtume	• Jipeleke mwenyewe polisi kwa dhuluma uliyotekeleza na uweze kuwajibikia matendo yako kwa mujibu wa sheria. • Haki ni sehemu muhimu ya kuyajenga upya maisha yako na maisha ya manusura na huenda ikachukua mfumo mwingine zaidi ya unaotakiwa na sheria ya nchi.

Kile watekelezaji wanaweza kufanya	Jinsi hili linavyoonekana ki matendo
Patana/Fidia	• Lipa fidia kwa makosa uliyoyafanya. Kwa mfano, rudisha pesa ambazo ulikuwa ukimnyima mpenzi wako, au ambazo hukuwa unazitoa kwa ajili ya watoto wako. • Kubaliana na mtu wako mwajibikaji*** hatua utakazochukua kuleta upatanisho na jinsi utakavyozichukua hatua hizo. • Jitoe uwajibikie maagizo ya kila wiki na utoaji ripoti kwa uaminifu. • Wakati wote mweke manusura katikati ya hatua hizo na mpatanishi amuulize kile anachohitaji kutoka kwako.
Andika	• Andika yale makubaliano yaliyowekwa na mtu wako wa uwajibikaji na mikutano iliyokubaliwa kusasisha juu ya hatua uliyochukua kubadili mtazamo wako na tabia yako mwenyewe. • Usitoe vijisababu au kujitetea kwa kutochukua hatua mlizokubaliana. • Wajibikia kikamilifu wewe mwenyewe na uoneshe jinsi mtazamo na tabia zako zilivyobadilika.
Pitia tena	• Pitia makubaliano yaliyowekwa kila baada ya muda maalum ili kuhakikisha kuwa yanafuatwa waziwazi kwa ajili ya mabadiliko yanayohitajika kuzuia kutokea kwa dhuluma zaidi. Unaweza kukubaliana na mwenzi wako wa uwajibikaji kuhusu vipindi au muda huu maalum na unaweza kufanya hivyo kwa simu au kupitia intaneti wakati wa vikwazo vya COVID-19. • Usikiuke makubaliano ya kufanya tathmini na fuata tarehe na saa zilizokubaliwa na mwenzi wako wa uwajibikaji. • Wajibika na uyakubali matendo yako na utelekezaji wako mwenyewe. • Usimpakazie mwingine matendo yako, usikane dhuluma, usiidunishe dhuluma uliyotekeleza, usitoe vijisababu vya kutetea tabia yako au kumlaumu mtu mwingine kwa matendo yako.

**** Watu wa uwajibikaji wanahitaji kuwa na busara sana kwenye vipengele tofauti vya dhuluma ambazo mnyanyasaji anaweza kutumia ili kupata nguvu na utawala. Mara kwa mara watekelezaji wa dhuluma wanaweza kuwa wachangamfu na washawishi na wanaweza kumpamba mtu vizuri. Sharti kuwe na werevu wa akili na kutokubali vijisababu na uteteaji wa dhuluma zao na kwa kutochukua hatua iliyokubaliwa au kukiukwa kwa makubaliano yaliyoafikiwa. Hilo linahitaji sheria kali na mwongozo.*

Utetezi

Utetezi ni kusema kwa niaba ya wengine, pamoja na wengine na kwa niaba ya wengine kuangazia udhalimu au pengo katika utoaji wa huduma ambao unaweza kuwa na athari kwenye sehemu moja ya jamii na kuwaacha wakiwa chini. Kutetea kwa niaba ya wengine haswa wakati huu wa janga, huwezesha serikali na makanisa kuona mapungufu katika kuyashughulikia na kufanya kazi ya kuziba mapengo hayo.

Ni muhimu kila wakati kuwa na heshima katika kuwasiliana na viongozi wa makanisa na viongozi wa serikali. Hakikisha kwamba unaelezea wazi suala ambalo unawasiliana nao kwalo, athari zilizoko kwako wewe mwenyewe, nyumbani, katika jamii n.k, na kile unachokiomba kama suluhisho linaloweza kutatua suala hilo.

Ikiwa inawezekana, na ni salama kufanya hivyo katika nchi yako mwenyewe, fikiria kuhusu kupeleka utetezi wako kwa ajili ya mambo yafuatayo:

Omba:

1. Upate ufadhili wa huduma za dhuluma za nyumbani kadri mahitaji yanavyoongezeka.
2. Upate ufadhili wa nyumba salama/makimbilio kadri mahitaji ya wanawake na watoto kulindwa kutokana na madhara yanavyoongezeka.
3. Upate kampeni ya matangazo ya kitaifa inayoangazia suala la dhuluma za majumbani na mahali pa kupokea msaada wakati wa janga la kimataifa.
4. Kuwe na utekelezaji wa sheria ambazo zinafanya dhuluma iwe ni kosa la jinai ili wahalifu waweze kukamatwa na kushtakiwa.
5. Kuwe na elimu ya kimfumo ya polisi na mahakama juu ya dhuluma za nyumbani zinavyotegemea jinsia na kuenea kwake na athari zilizoko ili waweze kushughulikia hali hiyo kulingana na utendaji bora wa kazi.
6.

Muhtasari

Kumbuka dhuluma za nyumbani hutokea, ikiwemo makanisani..

Tazama uone dalili za dhuluma na ukabiliane nayo kwa mfumo wa TIMA – Tambua, Ikitia, Mtume na Andika kwa ajili ya mnusurika.

Wafanye watekelezaji dhuluma wawajibikie matendo yao na wahimize wafuata zile hatua saba za – Tambua, Tubu, Ondoa, Mtume, Patana, Andika, Pitia huku wakikubali kwamba upatanisho silo lengo -lengo ni kusimama kidete kuhakikisha manusura yuko salama, yuko katika hali nzuri kiakili na anapewa hadhi yake.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho cha Kwanza
Rasilimali na Viunganishi

Nambari za Simu Ulimwenguni zinazohusu msaada kwa Dhuluma za Nyumbani hotpeachpages.net

An equity based approach in dealing with the pandemic – Men Engage Alliance menengage.org/resources/an-equity-based-approach-to-dealing-with-the-covid-19-pandemic

Men in Lockdown
restoredrelationships.org/Men_in_Lockdown

Men under Pressure
restored.contentfiles.net/media/assets/file/Advice_to_Men_in_Isolation_2020_v2.pdf

Malaysia Women's Aid
wao.org.my/implement-emergency-response-to-domestic-violence-amid-covid-19-crisis

Rasilimali za mwitiko wa Restored COVID-19
www.restoredrelationships.org/Covid19

Church Pack on Ending Domestic Abuse in English, French, Spanish, Portuguese, Arabic, Russian, Swedish, Polish and Hindi
www.restoredrelationships.org/resources/info/51/

Church Pack on Ending Domestic Abuse adapted for the USA www.restoredrelationships.org/resources/info/147/
Church of England's Domestic Abuse and COVID-19 resources

churchofengland.org/safeguarding/promoting-safer-church/domestic-abuse-and-covid-19

Making a Safety Plan
www.restoredrelationships.org/help/making-a-safety-plan/

Dhuluma za nyumbani: In Churches Too – UK research on domestic abuse amongst churchgoers across Cumbria infographic
www.restoredrelationships.org/resources/info/146/

Dhuluma za nyumbani katika Makanisa:
Peru
www.restoredrelationships.org/resources/info/83/

Argentina
www.restoredrelationships.org/resources/info/100/

Bolivia
www.restoredrelationships.org/resources/info/90

Redemptive Masculinities (Chitando and Njoroge 2016, Chitando and Chirongoma 2012)
archived.oikoumene.org/fileadmin/files/wcc-main/documents/p4/ehaia/RedemptiveMasculinities.pdf

Kuumbwa kwa Mfano wa Mungu: From Hierarchy to Partnership, World Council of Reformed Churches
wcrc.ch/wp-content/uploads/2015/04/CreatedInGodsImage.pdf

Kuumbwa kwa Mfano wa Mungu: From Hegemony to Partnership (positive masculinities manual), World Council of Reformed Churches
menengage.org/wp-content/uploads/2014/07/PositiveMasculinitiesGenderManual_0.pdf

Wiki nzima pasipo zana za dhuluma, World YWCA
worldywca.org/ywca_ressources/week-without-violence-toolkit-2019-is-now-available

Kiambatanishi 2

Takwimu za Dhuluma za Nyumbani na Athari Zinazotokana na Jinsia

Ukweli na takwimu kutoka UN Women kuhusu dhuluma dhidi ya wanawake:
unwomen.org/en/what-we-do/ending-violence-against-women/facts-and-figures

Bunge la Ulaya limeripoti kwamba dhuluma za nyumbani ziliongezeka kwa thuluthi moja katika baadhi ya nchi za Muungano wa Ulaya (EU) kutokana na kusitishwa kwa shughuli za kawaida (lockdown)
europarl.europa.eu/news/en/press-room/20200406IPR76610/covid-19-stopping-the-rise-in-domestic-violence-during-lockdown

Australia imeripoti ongezeko la 75% la utafutaji kwenye intaneti unaohusiana na usaidizi kwa ajili ya waathiriwa wa dhuluma za nyumbani.
france24.com/en/20200406-un-chief-decries-horrifying-rise-in-domestic-violence-amid-virus-lockdown

Uingereza ina ongezeko la mara tatu la mauaji ya kinyumbani katika kipindi cha wiki tatu za lock na asilimia ongezeko la 25% ya simu zilizopigwa kwenye nambari ya usaidizi ya kitaifa inayoshughulikia dhuluma za nyumbani.
In the UK, a Parliamentary committee heard that 14 women and two children had been killed in the first three weeks of the lockdown.

sarahmullally.wordpress.com/2020/05/01/loving-as-christ-loved-during-covid-19

Huko Malaysia, shirika la Women's Aid limeshuhudia ongezeko la 44% la simu zinazopigwa kwenye nambari ya usaidizi

.wao.org.my/implement-emergency-response-to-domestic-violence-amid-covid-19-crisis

Brazili imeshuhudia ongezeko la 50% la simu zinazopigwa kwenye nambari ya usaidizi kwa ajili ya dhuluma za nyumbani.

In Kenya, the National Council on Administration of Justice reported 'a significant spike in sexual offences in many parts of the country'.
hrw.org/news/2020/04/08/tackling-kenyas-domestic-violence-amid-covid-19-crisis

Huko Uingereza utafiti uliofanywa na University of Coventry na University of Leicester ulipata kwamba mtu 1 kati ya watu 4 ambao huenda kanisani huko Cumbria, jimbo la Uingereza, walikuwa wanadhulumiwa katika mahusiano waliyomo sasa. Idadi hii ilipanda hadi 42.2% wakati mahusiano ya awali yalipojumuishwa. Zaidi ya 90% ya dhuluma zilitekelezwa na wanaume
restoredrelationships.org/resources/info/146/

Utafiti uliofanywa katika makanisa huko Bolivia, Argentina na Peru ulionesha kwamba dhuluma za nyumbani zilikuwa zinatokea makanisani pia
restoredrelationships.org/resources/info/83/

Athari Nyingine

Kudorora kwa huduma za afya kwa kina mama
pewtrusts.org/en/research-and-analysis/blogs/stateline/2020/04/17/fearing-coronavirus-many-rural-black-women-avoid-hospitals-to-give-birth-at-home

Dhuluma ya Umma –

Ukatili wa polisi katika kutekeleza amri za kujitenga:

Across Africa
bbc.com/news/world-africa-52214740

India
dw.com/en/india-police-under-fire-for-using-violence-to-enforce-coronavirus-lockdown/a-52946717

Shukrani

Mwandishi

Mandy Marshall
Director for Gender Justice
The Anglican Communion

Wachangiaji:

Chiseche Mibenge
Episcopal Relief and Development, USA

The Revd Rachel Carnegie
Anglican Alliance

Paulo Ueti
Anglican Alliance and Anglican Communion Office, Brazil

Martha Jarvis
Lambeth Palace, UK

Andrew Khoo
Advocate and Solicitor, Malaysia

Sally Smith
Consultant, UK

Tagolyn Kabekabe
Anglican Alliance, Solomon Islands

Rob Dawes
Mothers Union, UK

Naomi Herbert
Mothers Union, UK

Provincial Community Development Coordinators
Mothers Union, Worldwide.

Esther Sweetman
Restored, UK

The Revd Carole Hughes
IAWN Member, New Zealand

The Revd Lizzi Green
IAWN Member, UK

The Revd Canon Dr Helen Van Koevering
IAWN member, USA

Published by the Anglican Consultative Council and the Anglican Alliance
Saint Andrew's House
16 Tavistock Crescent
London W11 1AP
United Kingdom

www.anglicancommunion.org
www.anglicanalliance.org

This resource may be used and copied without license, provided due credit is given to the author and publishers.

© 2020 The Anglican Consultative Council and The Anglican Alliance

Please note this document makes use of licensed stock photography.
All photography is for illustrative purposes only and all persons depicted are models.

ISBN: 978-1-913863-08-1